



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)



18/03/2025

**TANGAZO LA KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA KUOMBA MIKOPO YA 10%
INAYOTOLEWA NA HALMASHAURI KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA
NA WATU WENYE ULEMAVU**

(Limetolewa kwa kuzingatia kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2024 Kifungu cha 7 (1))

Mkurugenzi wa HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA anawatangazia wananchi kuwa dirisha la kuomba mikopo ya 10% kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu litafunguliwa tarehe **20/03/2025** na litafungwa tarehe **20/04/2025**. Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ina jumla ya Tsh **Mil. 251,096,291.29** kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Hivyo Mkurugenzi wa Manispaa anakaribisha vikundi vyenye sifa kutuma maombi yao kupitia mfumo wa kielektroniki. Vikundi vitakavyopewa mkopo lazima viwe vimesajiliwa na kuomba mkopo kupitia mfumo wa WEZESHA PORTAL (tembelea tovuti: www.mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz).

Sifa za vikundi vinavyotakiwa kuomba mkopo;

- i. Kikundi cha **WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU** kilichotambuliwa na kupewa cheti kwa mfumo wa kielektroniki.
- ii. Kikundi kiwe kinajishughulisha na shughuli za ujasiriamali au kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali
- iii. Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya watu kuanzi watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na watu kuanzia wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa

ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya manajimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake.

- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi
- v. Wanakikundi lazima wawe raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha kwa kikundi cha vijana wanakikundi wanapaswa kuwa na umri kunazi miaka 18-45

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (tovuti: ww.mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii au Afisa Mtendaji wa kata husika kwa maelekezo zaidi.

Tangazo hili limetolewa na;



Jacob S. Nkwera

**MKURUGENZI WA MANISPAA
BUKOBA**

MKURUGENZI WA MANISPAA
A MASHAURI WA MANISPAA
BUKOBA